SALA ZA MTU MMOJA

Mwongozo wakustawisha maombi yako

Mwandishi

NDUGU YOHANA-KAROLI, F.O.D.C.

2010

Haki ya mwandishi© Ndugu Yohana-Karoli, F.O.D.C.:

Hakuna kibali kitakachotolewa tena mara ya pili ama kupelekwa kwa namna yeyote ya elekitroniki au kupigwa chapa kwa mashine pasipo ruhusa kutoka kwa mwenye kutoa kitabu, isipokuwa kupitia mtu ule anayetaka kukagua na kuchagua kwa ufupi maandiko kwa ajili ya kuweka ndani ya gazeti.

Kimetolewa na
Wilkins Foundation, Inc.
untoallnations@charter.net

Kimetengezwa tayari kuchapishwa na
Jan Brown

Kilipigwa chapa Marekani

Kwa ajili ya Jan, rafiki mwema na katibu mwaminifu

Kimetolewa kwa YAKOBO BYRON KENYON, Ph.D. AICP
Aliyezaliwa Mayo 22, 1927
Aliaga dunia Novemba 23, 2009

KUHUSU MWANDISHI

Ndugu Yohana-Karoli alistaafu kwa kazi ya Askofu Mkuu wa kanisa ya Anglikana Katolika, sasa anakaa Maitlan, Australia. Kabla ya hapo Yohana-Karoli alikuwa Mtumishi mku katika kazi tofauti kulingana na utaratibu wa dini katika kanisa ya Anglikana Katolika. Alikuwa Askofu msaidizi na pia Kasisi mkuu katika jimbo la Australia kabla kutawazwa Askofu kwa desturi za kanisa ya Anglikana Katolika katika jimbo ya New Orleans. Hapo zamani alikuwa Askofu msaidizi wa Adelaide na kasisi mkuu katika Eyre Peninsula, Australia, wakati moja alikuwa Askofu katika Polynesi, pana siku alikuwa Askofu msaidizi wa kufanikiwa kwa Worcesta, Chelmsford, Southwark, huko Ulaya. Huko Marikani, aliwahi kuwa mwalimu wa Chuo Kikuu akifundisha Tewolojiya ya kujinyima anasa za mwili katika Seminari ya Nashotah, alikuwa Askofu msaidizi wa Quincy, na mushauri wa wanafunzi katika Seminari ya Holyrood, New York.

DIBAJI

Sala za mtu pamoja na kushukuru

Ni kwa mshangao na haya, nashirikiana maombi haya pamoja na nyi. Kwa miaka nyingi nilipata kujua ya kwamba jambo la kufaa na kuleta faida ni kuomba na kalamu mkononi. Watu kadha wanaona ni ajambo la maana kuomba kwa njia hiyo. Kulingana na imani yangu ya kwamba kitu chochote hakijadhihirishwa kwa maombi, ni kwamba bado hakijaeleweka wala kutakaswa wala kukombolewa ndiyo imenipa msukomo wa kuleta ufunuo huu mwenyewe kwa tumaini ya kuwa wengine huenda wafahamu kwa upana na kwa ndani jinsi ya kuzungmuza na Mwenyezi Mungu yeye binafsi.

Wakati huu sina uwezo ya kuingia Maktabani; kwa sababu hii, siwezi hakikisha maadondo yangu wala kuonyesha sawasawa chanzo chao. Kwa ajili hii, naomba huruma ya wenye vitabu vingine kwamba sija kataa kwa makusudi kushuariana na wao kulingana na maneno niliyotumia katika vitabu vyao.

+ Yohan-Karoli, F.O.D.C.
Askofu Mkuu na Kiongozi wa Kanisa la Anglikana Katolika

1

SALA KWA ROHO MTAKATIFU

Maombi Ya Kufanyika Upya

Bwana, leo kwa kupitia siri za hamsini baada ya Pasaka ulitakasa Kanisa lako miongoni mwa watu wote na mataifa yote. Tunaomba, mimina karama za Roho Mtakatifu wako juu ya ulimwengu wote na uendelee kufanya kazi ile ya upendo ndani ya roho ya waumini, jinsi ulivyoanza katika mahubiri ya injili ya kwanza. Amina.

Sala kwa ajili ya Roho Mtakatifu

Baba wa nuru ambaye kila karama nzuri inatoka kwake, tunaomba, tuma Roho wako ndani ya maisha yetu kwa nguvu za pumzi isioweza kuzuiwa na mtu au kwa mwali wa moto wa hekima yako, fungua fikra zetu. Fungua ulimi wetu hivi tuimbe sifa zako kwa maneno yapitao lugha za wanadamu, maana bila Roho wako hatuwezi paaza sauti yetu na maneno yenye amani au kutangaza ukweli kwamba YESU ni BWANA. Amina.

+ + +

Sitamani chocote kitokacho kwake Bwana, bali upendo wa Mungu ndiyo natamani, ninatazamia wewe tu. Bwana, chukua hili neno, na ufanye liwe hakika siku zote ndani ya moyo yangu, milele na milele.Amina.

+ + +

Sala Kwa Ajili ya Mabadiliko ya Ndani Kabisa

Mungu, Baba, na Bwana, unipatie neema kusudi nisitamani kitu chochote hivi niweze kufurahia vitu vyote; unijalie kusudi nisitamani majivuno ili niweze kufahamu vitu vyote; unipatie uhuru pasipo ubinafsi wala tamaa mbaya ya kitu chochote hivi nipende vitu vyote na watu wote. Bwana, unijalie, mapumziko na amani, utulivu halisi amani ya ndani kabisa ili nibadilike na kuepuka tamaa ya kujipatia mwenyewe, au ubinafsi, au kutawala, au uchoyo, ili uniweke huru kutokana na furaha ya uwongo nakufadhaika, huzuni, kusononeka moyoni, au hasara. Bwana, uhifadhi unyenyekevu wangu, unifanye hivi niwe msafi. Amen.

+ + +

Ninakushukuru, maana umekuwa roho mmoja ndani yangu, katika umoja bila machafuko. Hubadiliki na hugeuki, Mungu juu ya vitu vyote, tena umeendelea kuwa kila kitu kwangu: Chakula cha ajabu, umetoa bila kuzuiwa, unalisha moyo wangu kila mara; kisima kibubujikacho kwenye moyo wangu; vazi la nuru, moto unateketeza pepo mbaya, utakaso ule unaoniosha mimi msafi milele na machozi matakatifu yatatolewa wakati utakuja kutembelea watu wako wote. Amina.

+ + +

Ninakushukuru, maana kwangu Wewe ni nuru isiotambua usiku, jua lisilotua kamwe. Nakuomba sasa, angaza moyo wangu. Wewe huwezi kujificha, kwa kuwa utajaza vitu vyote na utukufu. Wewe hujifichi kwa mtu yeyote, lakini kila mara sisi tunajificha kwako. Ee! Ujinga mkubwa! Tunajificha na hatutaki kukukaribia Wewe. Tunaweza kujificha wapi hata hatuna mahali pa kupumzika? Au, kwa nini tunataka kujificha na bado tunaishi pamoja na watu wote na hatuogopi mtu yeyote? Amina.

+ + +

Simamisha hema lako ndani yangu, Bwana wa rehema, tengeneza makao yako ndani yangu sasa hivi na uishi daima ndani ya mtumishi wako pamoja hadi mwisho. Mara nikiondoka katika maisha ya ulimwengu huu na baadaye niweze kupatikana ndani yako na nitawale pamoja nawe ee Mungu aliye juu kupita vitu vyote. Kaa nami, Bwana, usiniache pekeyangu. Maadui wanaonitafuta kila mara kuaangamiza nafsi yangu, wakipata Wewe uko ndani yangu utawakimbiza ndivyo hawatapata mamlaka yoyote maishani mwangu, wanapokuona ndani yangu ee Mwenye nguvu, mwenye nguvu kushinda wao wote, ambaye unaishi ndani ya moyo wangu. Amina.

+ + +

Bwana, Wewe hujanisahau kamwe, ijapokuwa nilikuwa katika maisha ya ulimwengu na kuangamia kwa kutojua, ulinichagua ukanitenga mbali na ulimwengu na ukaniweka katika uwepo wa utukufu wako. Unihifadhi thabiti na nisidhoofike kwenye makao ya ndani uliyeumba nafsini mwangu. Amina.

Ijapokuwa nimekufa, ninakaa nikitazama Wewe tuu. Wewe ni wangu, ingawa mimi ni maskini, mimi ni tajiri kupita mtawala yeyote.

Kukumega na kukunywa Wewe, kujificha ndani yako kila siku, nitajaliwa baraka na furaha zaidi maana Wewe ndiye baraka zote na fahari zote na shangwe na utukufu viwe kwako.

Utukufu kwa utatu takatifu asili ya upaji uhai, wakuabudiwa na Watakatifu wanakiri na kusujudu katika Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu sasa na kizazi kwa vizazi vyote. Amina.

+ + +

Mungu, Wewe ndiye ulituumba sisi.
Ee Mungu, Wewe ndiye ulitukomboa.
Ee Mungu, Wewe msaidizi wetu sasa.
Ninakusujudia na kukuabudu.

YESU,
Ukamilifu wa vitu vyote.
YESU,
Yesu kila mahali: sikuzote Yesu.
YESU,
YESU,
YESU,
Kwakukupenda, kwa kukutumikia.
Kutukuza jina lako katika umoja wa UTATU – hili ndilo jambo la maana.

+ + +

Baba ninaachilia maisha yangu mkononi mwako ili ufanye jinsi mapenzi yako yalivyo. Chocote utafanya, nitakushukuru. Niko tayari kwa yote; nakubali yote. Acha mapenzi yako pekee yafanyike maishani mwangu na katika vyote. Bwana, sitamani kupita hapo, Ee Bwana. Naweka nafsi yangu mkononi mwako. Natoa upendo kutoka kwa moyo wangu huu dhaifu, natoa yote kama dhabihu kwako, maana nakupenda, Bwana, kwa njia hii nataka kutoa nafsi yangu, nijisalimishe mkononi mwako pasipo kupunguza upendo wa moyo wangu huu dhaifu na matumaini bila mpaka, maana Wewe ni Baba wangu. Amina.

+ + +

BAADHI YA MWONGOZO KATIKA NJIA YA MAOMBI

Maombi yanaweza kuwa katika njia ya maneno, nyimbo, mashairi, na wakati wa kukaa kimya. (Angalia Zaburi 86, 88, 19, na 23.) Upendo ni shina ya maombi halisi, unaanza na maneno, lakini maneno ni machache mno, na neno lenye sauti moja tu.
Kimya – Zaburi 108
Tafakari – maombi ya fikra nyingi
Katika kuwaza
Kutumia akili unapo tafakari
Kufuata neno la Biblia
Tazama – na upendo, tambua kwa uangalifu na jibu kwa Mungu, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.

Baada ya muda kidogo, na katika muda wa kuanza, maneno yanakuwa mengi zaidi hata karibu kupinga hali ya maombi. Sasa tunaweza kuiingia kwenye maobi mafupi. Moyo unakuwa pamoja na Mungu sehemu ya pili, ni kama kutazama na macho ya upendo, kwa kusudi moja pekee.

Hapo tunaweza kuwa pengine na ukavu, giza, na hata kuteseka kiroho. Msaada unaweza kupatikana kupitia kwa sala za kuomba kupitia kwa maombi ya kasisi na watu wakikusanyika pamoja, maombi ya kurudiarudia, maombi ya Rozari, na kwa watu wengi. Maombi mazuri kuliko mengine ni Sala ya Bwana. Wakati huu unaweza kuwa muda maalum wakupanda kiroho ikiwa tutajisalimisha na tegemeo letu liwe kwake Mungu, na ikiwa tutaweka kando kwa muda mawazo ya jambo lisiloeleweka kuwa kweli ambayo hayawezi kusaidia kamwe wakati huu wa kuendelea kuwa katika maombi. Sisi….

…….tunapoteza jaribu la kulenga vitu halisi. Tunaweza onekana tumetupwa. hakuna faraja. Usikate tamaa, huu unaweza kuwa mwanzo wa maombi mapya ya ndani kabisa. Huu ni wakati wa kuitikia amri: "Simama imara ujue ya kuwa MIMI NI MUNGU." Kwanza tunapitia hali ya kutamani kukuwa ili Roho Mtakatifu atuongoze, na kututuliza kwa Mungu pekee, ili tuweze kuruhusu upendo wetu kufikia baraka za Utatu takatifu. Tunasubiri tupate amani hivi tujibike. Mungu ukutana nasi, na tunapumzika ndani yake.

Maana njia ni maombi yenye kutoka ndani, angalia Yohana 14:15, 14:21, na 14:23. Mungu atuzidishie sisi kwa nguvu za upendo wake na kwa maisha yake, kwa urafiki wa kipekee. "yote yataenda kuwa mazuri na desturi ya vitu vyote itakuwa njema."

+ + +

Mungu, Baba wa sote, juu ya wote, kushinda wote, naamini kwamba Wewe ni mpya kila asubuhi. Njoo uzaliwe ndani yangu leo hii. Naamini yakuwa kila mara Wewe hujishugulisha na kazi yako ya umuumbaji katika ulimwengu wako. Fungua moyo wangu na fikra zangu ili niwe tayari kupokea siku kwa siku katika uumbaji wako. Wewe ni wa wakati huu. Fanya nifahamu, hata ukitenda mambo ghafula sitakuwa na mshangao. Unisaidie kugundua kila mara kwamba Wewe ni mshangao wa ajabu kupita vyote. Sisi si wafungwa wa ulimwengu huu, Wewe uko pamoja nasi, karibu sana nasi. Amina.

+ + +

Unakaa ndani yangu, kwa siri, mpendwa siku zote. Ninaamini ya kuwa Mungu Roho Mtakatifu anatenda katika kanisa sasa, katika ulimwengu, na kwa sehemu yangu yote. Yeye ni roho wa uumbaji na mimi ni kiumbe kipya.

Mungu, Baba, mimi niko hapa pamoja nawe, Baba – Baba na Yesu – Baba yangu, upendo wa Baba, upendo wako kwa ajili yangu. Baba Mwenyezi, Wewe uko hapa pamoja nami; siko pekeyangu. Wewe uko hapa, Baba, ukweli wote – hapa pamoja nami. Mpendwa kabisa – Mtakatifu hapa, Mungu, yote-hapa, na sasa. Siku zote pamoja nami, pamoja nami – mwenye dhambi, muasi, mpotevu na nimepatikana – Alleluia! Nakutamani, na Wewe uko hapa sasa na hata milele. Amina.

+ + +

Kijana wa Mtu mwenye cheo kikubwa

Yesu, Mfalme, mimi ni kijana / binti wako. Tenda ndani yangu- kwa ajili yangu – Bwana wa wote. Mimi ni mwanao nimepata hasara kwa ujinga wangu na kutotii kutokana na tamaa zangu za haraka – moyo umevunjika, nimetengwa mbali.

Bwana, naamini; nataka kuamini kwa nguvu zaidi, kwa uaminifu zaidi. Chochea imani yangu wacha ichipuke chemichemi ya utiifu maishani mwangu. Wewe utaponya na utarudisha sasa. Sifa kwako, Bwana. Nakushukuru kwa kuniponya na kwa ajili ya uzima. Wewe ni mponyaji wa yote, mwenye kurudisha vyote. Kwa sababu Wewe ndiye mwenye kutoa vyote, na kwa niaba yako mwenyewe unatugawia vitu vyote bure Baba, dhihirisha utukufu wako ndani yangu. Angaza ndani yangu; Angaza popote katika mtumushi wako. Amina.

+ + +

`

Birika ya Bethzatha

Mwanaume huyu kama mimi ambaye amekuwa hajiwezi alikuwa amefungwa na hofu tena na kushindwa a mengi. Kwa hivyo, ameshindwa kuliko wengine, na ni muzigo kwa wengine. Hata mimi pia ni baadhi ya mambo kama haya sasa, ninaomba, unifungue. Naweza kubeba mizigo yangu pamoja nawe Yesu na nguvu zako. Kubeba mizigo ni ishara ya uponyaji na kufunguliwa. Amina.

+ + +

Utakatifu wa Mungu

Bwan Mungu uliye hodari, dhihirisha asili yako yote na udhaifu wangu mwenyewe. Sina kitu; mimi sikitu; siwezi kufanya chochote. Unisaidie kutamani, kuliko yote, nifanyike Yerusalemu, Mji Mkuu wa amani, nataka kukuwa nawe Yesu wa baraka kwa amani, na upendo.

Ni lini nitakupenda, Bwana, na upendo unaokustahili? Ni lini nitakupenda jinsi Wewe unavyonipenda? Unifungue katika upendo wa unafiki, ili niweze kukupenda Wewe kabisa. Amina.

+ + +

Baba, ninajiachilia kabisa kwako: fikra zangu na kuwaza kwangu, ulimi wangu wa kusema, mwili wangu wa kufanya kazi, na hali yangu ya mapenzi vipate kutakasika na kuridhika. Matendo yangu ya kale nimeacha. Wakati wangu ujao ni wa tumaini. Sasa ninaishi kulingana na wakati huu. Takasa dhamiri yangu. Tia nguvu akiri zangu. Uimarishe madhumuni yangu. Ongeza imani yangu kwa njia kubwa. Penda upendo wangu kama dhabihu. Bwana niko hapa kwa mapenzi yako. Amina.

+ + +

KAZI YA MUNGU NA KAZI YA MWANADAMU

Nayafanya yote kuwa mapya; Yesu Kristo ndiye upya *Ufunuo wa Yohana 21:5*

Bwana, maisha mapya, ninatoa kwako, mimi mwenyewe kama vile niko karibu kufanyika upya kwa mfano wako na taswira yako, ili nifanyike hivyo hali ya kufanyika upya, ambaye ni mimi mwenyewe, upya katika ubatizo, nimefanyika upya katika imani nakatika ushirika mtakatifu wa Wakristo, upya kila siku jinsi mapenzi yako yalivyo, upya kila wakati. Alleluya! Uzima ni furaha ya ajabu.

Ni vyema kuwa hai, Mpenzi wangu Bwana, kwa sababu ni mpya siku zote Wewe ni upya, na kwa neema Wewe unaweza kunifanya upya. Amina.

+ + +

Bwana, upendo ni wa ajabu, na unatuletea mambo ya furaha, kwa vile tunapitia kwenye mambo mageni ambaye ni muchanganyiko wa furaha na uchungu, katika hivyo kuna uwezekano wa kutenda mambo ya kishetani. Wewe ni MPENZI wangu – hicho ndicho kitu bora! Ninataka kushikilia hapo. Natamani maisha yangu yote yafanyike kwa mutindo huo. Naona upendo wako hapa na hata sasa hivi: upendo wa utulivu wa wazazi wangu ambao unaendelea; uangalifu na kushugulika wa dada na ndugu zangu; upendo wa wapwa zangu wa kike na wa wapwa zangu wa kiume; upendo wa kudumu kutoka kwa marafiki wa zamani na wa sasa katika jamii ya Franciscan. Katika hayo yote ni upendo wako imenigusa na kupitia mimi ili niguse wengine – wale wadogo wanaosumbuka zaidi, wale watoto wao walijitoa kiroho, wale walinihudumia na kunisaidia sehemu nyingi. Bwana, Wewe hutoa karama ya upendo ili tugawane. Utusaidie kutoa na kupokea kwa ukarimu, na kwa utakatifu. Amina.

+ + +

Bwana, mapenzi ya nafsi yangu, ya mwili wangu pamoja na nguvu zake zote, unanipenda jinsi nilivyo: Bwana wa uhai wote; Bwana wa maisha haya; Bwana wa ulimwengu wote; Bwana wa sehemu hii kidogo; Bwana mwwenye hodari mno; kiongozi wa ustadi, muziki, mashairi na usemi wa kawaida; yule mpendwa kabisa. Unijalie baadhi ya uzuri huo, uwezo, na utakatifu ambavyo ni vyako. Kaa ndani yangu, angaza nuru yako ndani yangu, na uguse nafsi nyingine kupitia mimi. Niko hapa: nichukue, nitumie, na unibariki. Kama inawezekana univunje. Bwana, niko hapa. Unisaidie niwe hapa kwa ajili yako sasa! Amina.

+ + +

SIFA

Sifa ni njia yangu bora ya kuitika kwa wema wa Mungu na ukamilifu wake. Jinsi ninavyotazama ukuu wa Mungu na uzuri wake, yote ni shukurani yangu kwake Mungu mwenyewe; sifa zangu kwa Mungu mwenyewe; kanuni yangu kabisa kwa ajili ya Mungu; ni heshima yangu kubwa kueleza furaha yangu kwa Mungu. Hii ndiyo njia hakika ninayo ya kuelewa katika ufahamu wa ndani wa ubinadumu wa Mungu, asili ya Mungu, na maongozo ya Mungu. Njia halisi zaidi ya kujitawala ustawi wangu kiroho kwa huruma na neema ya Mungu ndiyo kujisikia vyema kutoka ndani ya moyo wangu mwenyewe kwa ajili ya Mungu. "Sifa kwa mtakatifu wa watakatifu aliye juu na kutoka ndani ya moyo, pokea sifa" (Oremus Hymnals).

+ + +

Sifa kwako, Bwana Mungu Mwenyezi, kwa ajili yako na kwa jinsi ulivyo. Utukuzwe Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, ndani yangu na kupitia kwangu, kama ilivyo mwanzo, pia sasa na milele. Amina.

+ + +

Heri, utakatifu, Utatu usiogawanyika, Mungu mmoja, Baba, Muumba, Mwenye kuhifadhi, Abba, Mwokozi, Ndugu, Mpendwa, Rafiki, Bwana harusi, na mke na mume, mwenye nguvu zote za uombezi, Roho, Kiongozi, mwenye kutakasa, Utatu wa milele ambaye uko sasa, ulisema na ikafanyika. Uliamuru na ikafanyika, na ikasimama haraka. Umebeba vyote. Unaendesha vyote kulingana na mapenzi yako. Amina.

+ + +

Wewe ni upendo. Wewe ni uhai na uhai wote unatoka kwako, na Wewe ni chanzo cha ukweli wote. Wewe umejaa utukufu wote, mwenye nguvu zote, umejaa utakatifu wote, umejaa wema wote, Mungu Mkuu, Mungu aliye hai na wa kweli, mwenye haki na usawa, mwenye huruma na rehema. Unahukumu bila ubinafsi. Ndani yako hakuna kurudi nyuma wala giza wala hubadiliki. Njia zangu sio njia zako maana Wewe uko hapa sasa na siku zote ndani yangu, pamoja nami, na kwa ajili yangu. Mawazo yako sio mawazo yangu, walakini Wewe huniwaza kwa upendo. Amina

+ + +

Mungu Mtakatifu, Wewe ni upendo, Wewe ni uhai, na chanzo cha uhai wote. Asante maana Wewe ni amani, Wewe ni wokovu, na mapumziko.

Moto unaoteketeza, upepo inaogawanya, tetemeko la kutikisha, Sauti ndogo ya utulivu, linda wote. Ongoza, elekeza, endeleza fikra njema. Mnenaji wa ukweli, nguvu za kitendo chema, mwanzo wa utakatifu na neema, ghala ya ukweli wote, ufunuo wa ukweli, na mwenye kutoa upendo. Amina.

+ + +

Sifa kwa Mungu yeye aliye mlima utokao moshi, musitu unaoteketea, Mtakatifu, Hodari, Mtulivu, Mukunjufu, Usalama wa kweli pekee, Mtakatifu aliyejaa heshima na kutisha. Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Wewe ni Baba Mungu wa Sabato, mpendwa sana, kilima cha utakatifu. Ua nzuri la bonde, marashi ya Sharon, hema la kupendeza sana, Makerubu na Maserupi waliabudu na kusujudu mbele zake, malaika na malaika mkuu na jeshi lote la Mbinguni wanaanguka chini kusujudia na sifa isio na mwisho. Katika Yeye sisi pia tutashangaa kwa kustaajabu, upendo na sifa zake. Kisima cha baraka zote, mwanzo wa jamii zetu za wanadamu, chanzo cha uponyaji wote, kiongozi mwenye fadhili. Amina.

+ + +

Umeguswa na udhaifu wangu, unavumilia uchungu wangu, mponyaji wa ugonjwa wangu, anayenisamehe dhambi zangu, anayerudisha afya yangu – sasa, wakati huu utafika. Amina.

+ + +

Nakupenda – mwenye huruma yote, nzuri – mwenye huruma yote, nzuri kabisa. Sifa kwako, Bwana Mungu, kwa ajili Wewe ni Mungu. Jinsi ulivyo, kwa sababu ya matendo yako ndani yangu, na katika mimi, na kwa sababu ya vitu utanitendea bado, na kwa sababu ya mambo unanitendea sasa hivi. Amina.

+ + +

Bwana Mungu, maadam, Wewe unaniruhusu, na kwa hivyo niko, nafsi yangu inaweza kufanyika nzuri. Wewe niko kama ulivyo, jinsi utakavyokuwa. Amina.

+ + +

Nakushukuru, Bwana Yesu, Ulinifia, ulikufa, ulizikwa, ukafufuka. Nakushukuru kwa sababu ya Msalaba, Mti wa utukukufu, kwa ajili ya wema wote, kila dhabihu, kila wakati njema ya upendo na huduma, kwa ajili ya uwezo mkubwa wa kuabudu katika ushirika mtakatifu wa kikristo, kwa ajili ya huduma ya kawaida, Kwa ajili ya ibada na sala za dini, mahubiri na kuungama, kwa sababu ya neema za kwanza kwa ubatizo, kwa sababu ya manukato ya uzima, kwa sababu ya upepo na bahari, na anga, kwa sababu ya nuru na giza, kwa sababu ya mvua na jua, moto, na theluji na kwa sababu ya nuru na giza, kwa sababu ya karama ya kimya na upweke, kwa sababu ya karama ya urafiki na ushirika, kwa sababu ya imani, tumaini, na upendo, kwa sababu ya upendo na haki ya wale wachanga. Amina.

+ + +

Yesu alisema “kuna mtu amenigusa: kwa sababu nimefahamu kwamba nguvu imenitoka” (Luke 8:46). Bwana, ninagusa Wewe sasa na hizi sifa zangu duni, na kutetemeka, kwa upendo na kutubu kwa hofu. Bwana, ruhusu na iwe hivyo, ruhusu amani yako na upendo wako vitiririke ndani yangu. Sifa kwako, Bwana. Bwana, nakuamini, nakuamini. Mungu Wewe uko pamoja nami sasa, dumu katika sifa zangu, Wewe uko karibu kuliko kuvuta pumzi, karibu sana kuliko mkono na mguu. Mungu aliyeniumba kwa ajili yake mwenyewe. Nimetoka kwa Mungu. Mimi ni mali ya Mungu. Naenda kwa Mungu. Mungu ananijua kabisa. Mungu ananipenda kabisa. Mungu ameweka huduma kwa ajili yangu – hapa, sasa, milele na milele. Amina.

+ + +

Simama kwa dakika chache na ufikirie juu ya jambo yafuatayo:

Msalaba – tumaini letu peke.
Ufufuo – uzima wetu mpya.
Pentekote – roho anaye maskani yake ndani yetu.

+ + +

Nakushukuru, Bwana Mungu, kwa sababu ya Msalaba, ufufuo, karama ya roho, sikukuu ya kupaa kwake Yesu Kristo Mbinguni, ubatizo, ushirika mtakatifu wa kikristo, toba, imani ya katoliki, amani ya ndani, amani katika ushirika, kwa uzuri wote na upendo wote na kupendana, upendo uliyotolewa kwa ajili yangu, upendo wote nimepeana; waalimu wote, wachungaji wote, na wafadhili. (*simama kwa dakika chache na taja majina yao katika hali hii ya maobi*).

+ + +

Nakushuru kwa ajili ya karama ya uzima, kwa maana ya uhai wote umenijalia (*simama kwa dakika chache na hesabu baraka zako katika hali hii ya maobi*). Nakushukuru kwa sababu ya karama ya mwili, akili, na roho. Nakushukuru kwa ajili ya siri za ajabu za mwili na roho na kwa sababu ya muujiza, urembo wa mwili wa mwanadamu. Nakushukuru kwa ajili ya Mashemasi na watu ambao si wahudumu katika ngazi ya juu kanisani. Nakushukuru kwa baraka ya Mungu juu ya wahuduma wetu, kwa ajili ya wale wanaofariji wengine, wanaotuongoza na wanaotufundisha sisi, kwa ajili ya wale wanakuja kwetu kutafuta ushauri, kwa ajili ya mwongozo, na toba. Amina.

+ + +

Ninyi Watakatifu wote wa Mungu, muombe kwa ajili yangu; ninyi malaika wote wa Mungu muombe kwa ajili yangu na kunilinda mimi, Malaika mtakatifu mlinzi wangu, kila mara nimekusahau na kukupatia huzuni, nisamehe na uniombee ili niwe imara katika vita. Amina.

+ + +

Roho Mtakatifu, Bwana mwenye mpaaji uhai, ulimzingira Bikira Mariamu mwenye neema ili yeye apate kuwa mama wa Bwana na mwokozi wetu Yesu Kristo. Shukrani zote ziwe kwako.

Naomba kwamba utafanya kazi kwa njia ya kisiri ndani ya moyo wangu jinsi ilivyo hali yake Yesu ya ukombozi na kukomboa jamii ya wanadamu wote. Naomba unijalie sehemu ya moyo wake Yesu ya upendo hivi niweze kuteketea na upendo kwa ajili ya Mungu Baba na kwa ajili ya wanaume na wanawake wote. Unijalie sehemu ya furaha yake na huzuni yake Yesu, kutaabika kwake Yesu na uwezo wake, na utumishi wake Yesu kwa ajili ya kuokoa ulimwengu.

Ruhusu Mariamu mwenye heri miongoni mwa wanawake, mama wa Bwana, uniombee ili Kristo afanyike ndani yangu, hili niweze kuishi kwa umoja na roho na hiari pamoja na Yesu Kristo, Mungu halisi na Mtu halisi, Mwanawe, Bwana na Mwokozi wetu. Amina.

+ + +

Uniongoze, Bwana, kutoka kuzaliwa hadi maisha mapya, kutoka kwa uongo hadi ukweli, kutoka kwa kukata tamaa hadi tumaini lenye kuniweka huru, kutoka kwa hofu hadi imani kamili, kutoka kwa chuki hadi upendo wenye ukarimu, kutoka kwa vita hadi amani. Achilia amani, amani yako, ijaze mioyo zetu, ulimwengu wetu, dunia yetu. Amina.

+ + +

Bwana wetu Yesu alisema, "kuwa huru ndani yangu, kwa ajili yangu, katika mimi."

Puliza ndani yangu, Roho Mtakatifu mwenye heri ili niweze kufikiria fikra zenye utakatifu; na uzidi kunijaza Roho Mtakatifu ili niweze kutembea katika ukweli zaidi kwa njia ya Yesu na matendo yangu yote yaweze kuwa matakatifu. Unikaribishe mimi, Roho Mtakatifu ili niweze kutazama Baba na kungaa. Unilinde Roho Mtakatifu ili niweze kulinda vitu vilivyo vitakatifu. Unihifadhi, Roho Mtakatifu, ili nisipoteze karama yako ya utakatifu. Amina

+ + +

Njoo, Roho Mtakatifu, na unijaze mimi pamoja na watu wa Mungu wote. Chochea ndani yetu zaidi na zaidi moto wa upendo. Chukua roho wangu, Bwana Mungu, Yesu Kristo, maana siwezi kulinda badala yako. Yesu, Bwana, wakati watu wameniona na kunisikia, acha wakuone na wakusikie wewe. Alleluya. Amina.

+ + +

Bwana Mungu wangu uliye mwema; unipatie upendo nyingi kwa ajili yako, kwa ajili yako mwenyewe peke. Chukua kile unataka, lakini uniweke mimi karibu na wewe.

Zidisha ndani yangu upendo kwa ajili ya Yesu, Mwana Wako, Bwana wangu na Mwokozi wangu, na kwa ajili ya Bikira Mariamu mwenye heri, mama wake na wangu, na kwa ajili ya majirani zangu walio karibu na walio mbali, kama vile nimeumbwa kwa sura na mfano wako. Bwana, Mungu, kwa rehema yako unisikie. Amina.

+ + +

Bwana, Mungu, unijalie Roho Mtakatifu wako katika nguvu zenye utukufu na kwa ndugu na dada zangu katika kanisa la Anglikana Katolika kwa uhai wetu, na maombi, na huduma. Utupatie maono ya mapenzi yako na ujasiri wa kukubali mabadiliko ambayo yatakupendeza Wewe ndani yetu.

Nakushukuru kwa ajili ya vitu vyote umetupatia mpaka sasa hivi na kwa ajili yakutuondoa sisi katika uoga wetu, utujalie neema ya kukubali chochote utahitaji.

Bwana, weka dada na ndugu zangu wote kwako. Unipatie na pia uwapatie njaa na kiu bila mwisho ili tuweze kutoa maisha yetu wenyewe kwako na ili tuweze kukuwa kikamilifu kwa njia ya utiifu kwa Yesu Kristo Bwana wetu, na kwako, Baba, katika yeye na katika Roho Mtakatifu, heshima yote na utukufu wote viwe kwako. Amina.

+ + +

Bwana, tuma Roho Mtakatifu wako ndani ya mioyo yetu. Kila wakati aweze kuongoza na kutawala mioyo yetu kulingana na mapenzi yako. Ututumie nguvu na utuimarishe wakati wa mateso na katika ushindi.

Utukinge na utulinde kwa uwovu wote na kosa na utuongoze katika ukweli uliyo ndani ya Kristo Yesu Bwana wetu, aliye hai na anayetutawala pamoja naye ni Roho yule yule, Mungu mmoja, milele na milele hadi mwisho wa kizazi chote. Amina.

+ + +

Shukrani kwako, Bwana Mungu, kwa ajili ya kazi yako ndani ya vitu vyote, ukombozi, utakaso, na kwa ajili ya maandiko matakatifu kwa ajili ya sakaramento.

Shukrani kwako kwa sababu ya ushirika wa watakatifu, kwa sababu ya neema yote ya maombi, kwa sababu ya leo kama bado mchana, kwa sababu ya leo hii ambaye ni siku moja tuu tunayo daima, kwa sababu ya sasa na hapa. Naomba neema ili niweze kutumia wakati huu vizuri na kukubariki mahali hapa.

Shukrani kwa ajili ya usingizi, nyumba, chakula, nguo, na burudani. Shukrani kwa ajili ya heshima katika huduma umenipatia ili niweze kuhudumia wengine, kwa ajili ya uzuri wa asili ndani ya wanadamu, katika ufundi, katika muziki, katika mashairi, kwa ajili ya vitabu na maandiko, kwa ajili ya baraka zote za maisha haya hapa na sasa, kwa sababu ya kuwa hai, kwa jinsi nilivyo, kwa ajili ya kazi ya Mungu, kwa ajili ya kanisa ya Anglikana Katolika, Kwa ajili ya mahali hapa, kwa ajili ya ibada ya leo, kwa ajili ya imani ya Katolika, kwa ajili ya viongozi wetu, kasisi wote wenye kuungamisha dhambi, madaktari wa meno, madaktari wakuu wote, madaktari wanaotibu miguu, muuguzi, na watunzaji wote. Amina.

+ + +

Mungu wangu, unisikie kwa ajili ya ukombozi na utakaso katika dhambi kupitia kwa Kristo Yesu katika nguvu za Roho Mtakatifu, Baba. Amina.

++ +

Baba, nakushukuru kwa ajili ya ufufuo wako, kwa ajili ya kumtuma Roho Mtakatifu, kwa utukufu wa Mungu Baba, kwa ajili ya ufufuo wa Bwana, kwa ajili ya siku ya Jumapili na ibada yake na ushirika, kwa ajili ya tumaini ya Mbinguni, kwa ajili ya uwezo wa kuabudu, kwa ajili ya ufunuo wa Maandiko matakatifu, kwa ajili ya maisha ya maombi, kwa ajili ya wahudumu na wale wamenihudumia mimi, jamii, marafiki, wafadhili, makasisi wenye kuungamisha dhambi, viongozi, madaktari, madaktari wa meno, madaktari wanaotibu miguu ya wanadamu, kwa ajili ya wale wote wanaonijali. Nakushukuru kwa ajili ya vitu vyote nilipata wakati wa utoto wangu na ujana wangu, kwa ajili ya mahali hapa, na sasa. Amina.

+ + +

Nakushukuru, Baba, kwa ajili ya upendo uliyofanyika mtu kupitia Bikira Mariamu mwenye heri maana ndani ya Yesu niko na tumaini, upendo, na uhai. Yesu, Bwana, Wewe ni tumaini langu, upendo wangu, uhai wangu, mabadiliko yangu. Nakushukuru, Bwana, kwa ajili ya maisha yangu. Amina.

+ + +

Tunakusifu, Mungu mwenye nguvu zote, kwa ajili ya Roho Mtakatifu na karama zake, kwa ajili ya wenye kuwa na ukweli, kwa ajili ya neema katika kanisa na ndani yangu, kwa ajili ya ubatizo, kwa ajili ya shahada, kwa ajili ya neema katika kanuni, kwa utakatifu, kwa ajili ya maisha yote ya utakatifu, kwa ajili ya maono, kwa ajili ya vitu vizuri mbele yangu, kwa ajili ya ishara zote za tumaini, kwa ajili ya uzuri ndani ya ua na ndege na anga, kwa ajili ya theluju na mwangaza, na jua, kwa ajili ya mvua, kwa ajili ya bahari na anga na nyota. Kwa ajili ya muziki, kwa ajili ya Maandiko matakatifu, na kwa ajili ya vitabu vya kiroho, tunakushukuru, Bwana.

+ + +

Mfalme wa Mbinguni, Mfariji wetu, Roho wa ukweli na upendo, Wewe uko kila mahali. Wewe hutujaza kila kitu chema. Wewe ni hazina ya baraka na mpaaji wa uhai. Karibu na kaa ndani yangu, unisafishe mimi kwa uchafu wote, na uniokoe na wema wako sasa na hata milele.

+ + +

Karibu, Roho Mtakatifu, njoo kama mwali wa moto, karibu Bwana, karibu Roho Mtakatifu. Fundisha ulimi wangu, angaza akili yangu, na fanya roho yangu iwe na nguvu wakati ninakutaka sana. Unifundishe mimi jinsi ya kunena juu ya Mungu na kwa ajili ya Mungu. Unisaidie kuabubu na ukweli kabisa, unionyeshe jinsi ya kuongoza nafsi za watu kwa Baba na kwa Wewe Roho Mtakatifu , na kwa Wewe Bwana Mungu, Roho Mtakatifu. Amina.

+ + +